Nuru ya Kiswahili, Juzuu 4(1), Juni 2025:115-142
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru41.115142

# Uchambuzi wa Mbinu za Ukwezwaji wa Wahusika wa Riwaya Pendwa ya Kiswahili: Mifano kutoka Riwaya ya *Njama* na *Kamata au Ua*

**Athumani S. Ponera**
**Profesa Mshiriki, Chuo Kikuu cha Dodoma**
athuman.ponera@udom.ac.tz

**Ikisiri**

Makala hii inachambua mbinu za ukwezwaji wa wahusika wa riwaya pendwa za Kiswahili. Ukwezwaji wa wahusika unajadiliwa kama mojawapo ya sifa bainifu za riwaya pendwa. Sifa hii inamaanisha kitendo cha kukipa kitu au mtu uwezo wa kiwango cha juu unaomwezesha kufanya jambo katika namna isiyo ya kawaida. Utafiti unaoripotiwa katika makala hii uliongozwa na Nadharia ya Umuundo inayojihusisha na suala la mjengeko wa matini (za kifasihi na zisizo za kifasihi). Data zilipatikana kwa njia ya kuchambua riwaya mbili zilizoteuliwa kimakusudi. Riwaya hizo ni *Njama* (1981) na *Kamata au Ua* (2020). Mbinu za ukwezwaji wa wahusika zilizobainika kutumiwa na waandishi wa riwaya teule ni: kuwavisha silika ya usangwini, kutumia sadfa, kuwavisha ujuzi wa juu wa kupigana, kuwapa uwezo mkubwa wa kufikiri, na kuwapa ujuzi wa hali ya juu wa kutumia teknolojia. Makala inapendekeza kuwa tafiti zingine zifanywe kuhusiana na vipengele vingine vya riwaya pendwa ya Kiswahili kama vile naratolojia, yaani sayansi ya usimulizi wa vitushi vya riwaya.

**Dhana za Msingi**: ukwezwa, riwaya pendwa, wahusika, umuundo

## Utangulizi

Riwaya ni kumbo mojawapo la fasihi (Njogu & Chimerah, 1999). Madumulla (2009) anaeleza kuwa riwaya huainishwa kwa kutumia vigezo tofauti. Vigezo maarufu ni fani, upeo wa kijografia, usimulizi, na maudhui.

Miongoni mwa aina za riwaya tuzipatazo kutokana na kigezo cha maudhui, kama asemavyo Madumulla (*ameshatajwa*), ni riwaya pendwa ambayo inajadiliwa katika makala hii. Urasimi wa riwaya pendwa unaangaziwa kuanzia miaka ya 1950 ulipoasisiwa na Muhammed Said Abdulla (kuanzia hapa na kuendelea tutamtaja kama MSA). Mkondo huu hujumuisha riwaya zinazovuta nadhari na kupendwa na watu takribani wa marika yote kutokana na kuwa na kiwango kikubwa cha usisimuaji. Kwa mujibu wa Madumulla (2009), sifa bainifu za riwaya za mkondo huu ni kuegemea katika maeneo ya mapenzi, ujambazi, mauaji, ujasusi, na upelelezi; kujichomoza zaidi kwa fani kuliko maudhui; kujengwa zaidi kwa msingi wa taharuki; kuvuma ghafla na kufifia ghafla; kuwa na u-mjini zaidi kuliko u-kijijini katika vipengele vya mandhari na maudhui yake; kutawaliwa na uharaka katika utunzi na uchapishaji; na kukweza wahusika wake (sifa inayojadiliwa katika makala hii).

Tangu ulipotambulishwa na MSA, kwa misingi ya kirasimi (tapo la sanaa ambalo husisitiza uandishi unaozingatia maadili ya kijamii na ya kidini), takribani miongo minane iliyopita (Madumulla, 2009), mkondo wa riwaya pendwa ya Kiswahili umepitia katika matapo mbalimbali. Katika miaka ya 1970 na 1980, mkondo huu ulizama katika tapo la ulimbwende (Mlacha & Madumulla, 1995). Hivyo, ulibeba sifa za jumla za sanaa ya kilimbwende ambazo, chambilecho Senkoro (1987), ni kupinga mikatale ya kirasimi (kama vile kuwa na mtindo rasmi, kutumia wahusika wenye sifa chanya tu, na kusawiri maudhui chanya tu); pamoja na kumpa uhuru kamili mwandishi (wa kuchagua mada, hadhira, na lugha) kwa kuzingatia matakwa yake. Sifa hizi ndizo zinazofanya kushamiri kwa riwaya pendwa kunasibishwe zaidi na kuzuka kwa tapo la ulimbwende. Mlacha & Madumulla (1995) na Madumulla (2009) wanayakinisha hoja hii kwa kusema kuwa, katika

muhula wa ulimbwende, ndipo ulishuhudiwa uchapishwaji wa riwaya nyingi zaidi zenye udaistopia, wahusika wawi (kama vile malaya, shetani, na majambazi), pamoja na maudhui yaliyovunja uzio wa kirasimi.

Miongoni mwa waandishi wa riwaya pendwa ya Kiswahili waliopeperusha bendera ya muhula wa ulimbwende ni Faraji Katalambula, Aristablus Elvis Musiba, Hammie Rajabu, na Mohamed (*Eddy*) Ganzel. Madumulla (*ameshatajwa*) anaeleza kuwa sababu za kushamiri kwa mkondo huu katika miaka ya 1980 ni mabadiliko ya kiulimwengu, ambapo jamii nyingi zilikuwa zinakabiliwa na ugumu wa maisha. Hivyo, sanaa pendwa (ikiwamo riwaya pendwa) ikatazamwa kama tabibu wa karibu wa mazonge na misawajiko ya kiakili, hususani ya watu wa mijini.

Mkondo wa riwaya pendwa ya Kiswahili ulijitokeza kwa kiasi kidogo kuakisi tapo la uhalisia, hususani kupitia kipengele cha maudhui. Madumulla (1993) na King'ei (1999) wanadokeza kuwa, licha ya kazi za mkondo huu kugubikwa na fani, baadhi ya waandishi—kama vile Faraji Katalambula na Hammie Rajabu—walisawiri maudhui yaliyojitokeza katika jamii bila kupindisha. Kwa ujumla, tapo la uhalisia halijapata uakisi wa kutosha katika riwaya pendwa.

Baada ya kumezwa sana na mwelekeo wa kilimbwende, mkondo wa riwaya pendwa ya Kiswahili ukakumbwa na nguvu ya tapo la usasa. Jumanne (2018) anabainisha kuwa tapo la usasa wa riwaya pendwa ya Kiswahili (na riwaya ya Kiswahili kwa ujumla) lilianza miaka ya 1990, kisha likashika kasi katika miaka ya 2000. Miongoni mwa sifa za fasihi ya usasa, kwa mujibu wa Khamis (2007) na Hacht & Hayes (2009), ni matumizi ya uhalisia mazingaombwe, muundo-geu (au muundo-pindu) uliokusudiwa, u-

ndotondoto, mitindo ya masimulizi isiyo ya kawaida, uhusika usiozoeleka, pamoja na matumizi makubwa ya teknolojia. Baadhi ya waandishi walioandika riwaya pendwa za Kiswahili za tapo la usasa ni Ben Mtobwa, Erick Shigongo, Hussein Tuwa, Patrick Kafuku, na Beka Mfaume.

Tumekwishaeleza kuwa sifa mojawapo ya riwaya pendwa ni kukwezwa kwa wahusika wake (wahusika wakuu na wale wanaowasaidia). Kwa mujibu wa TUKI (2001), dhana ya ukwezwaji inatokana na kitenzi 'kwea' ambacho kina maana ya panda (juu ya mlima au mti). Utendeshi wa kitenzi hiki unatupatia neno 'kweza'. Kwa muktadha wa taaluma ya fasihi, kukweza ni kitendo cha kukipa kitu au mtu uwezo au sifa za kiwango cha juu zinazomwezesha kufanya jambo na, hatimaye, kufanikiwa kulingana na lengo la mtunzi. Kwa mujibu wa Mlacha & Madumulla (1995), watunzi wa kazi mbalimbali za fasihi, zikiwamo riwaya pendwa, huwa na malengo wanayotaka kuyawasilisha kwa hadhira zao. Hapa, yanakusudiwa malengo kama vile kuelimisha na kuonya. Kwa upande wa riwaya pendwa, kama waelezavyo Mlacha & Madumulla (*wameshatajwa*), malengo yake yanayojichomoza ni kusisimua pamoja na kuwasilisha maudhui kwa ufanisi wa kiwango cha juu. Watunzi hutumia 'silaha' mbalimbali ili kufikia kilele cha shabaha hizo. Miongoni mwazo ni kuwakweza wahusika wao. Makala hii inachambua mbinu ambazo waandishi wa riwaya za *Njama* na *Kamata au Ua* wametumia kuwakweza wahusika wao.

Riwaya ya *Njama* ilitungwa na Aristablus E. Musiba na kuchapishwa, kwa mara ya kwanza, mwaka 1981 na Continental Publishers. Toleo hilo ndilo linalotumika katika makala hii. Riwaya hii inabeba sifa za msingi za riwaya pendwa ambazo zimekwishaelezwa. Madumulla (2009) anaonya kuwa, ili msomaji wa riwaya pendwa aweze kuelewa maudhui yanayokusudiwa,

inampasa awe makini sana. Hii ni kwa sababu mwavuli unaoifumbata riwaya hii ni fani inayopazwa na mbinu za hali ya juu za kipelelezi na za kimapigano. Ponera & Kasiga (2019) wanabainisha kuwa upelelezi na mapigano hayo yanafanyika baina ya makundi mawili ya wahusika—wahusika wema na wahusika wawi. Kundi la kwanza lina wahusika kama vile Willy Gamba, Veronika Amadu, Sherrif Amadi, Zabibu Abeid, na Eddy. Kundi la pili lina wahusika kama vile Chimalamo, Max, Shuta, na Sikazwe. *Njama* ni riwaya ya kimonolojia kwa sababu imetamalakiwa na usimulizi wa nafsi ya kwanza umoja. Sauti ya mhusika mkuu wa riwaya hii, Willy Gamba, ndiyo inayotawala katika usimulizi wa vitushi vyote. Kiini cha ploti ya riwaya hii ni upelelezi wa silaha za kisasa za wapigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika zilizopotea. Muhula wa kuchapishwa kwa riwaya hii ni wa ulimbwende ambao sifa zake tumekwishazieleza.

Riwaya ya *Kamata au Ua* imetungwa na Patrick C. Kafuku na kuchapishwa mwaka 2020 na Joystan Tanzania. Riwaya hii pia inabeba sifa mbalimbali za riwaya pendwa. Ploti yake imejengwa na upelelezi juu ya hila mbalimbali za kuhujumu rasilimali na ustawi wa nchi za Afrika Mashariki, ikiwamo Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Mhusika mkuu ni Mathew Mulumbi. Wahusika wengine ni Papii Gosu Gosu, Agai Sempa, na Ruby Rafael. Kwa kigezo cha usimuliaji, hii ni riwaya ya kidayalojia. Muhula wa kuchapishwa kwa riwaya hii ni wa usasa ambao sifa zake tumekwishazieleza.

## Kiunzi cha Nadharia

Utafiti uliozaa makala hii ulitumia Nadharia ya Umuundo. Nadharia hii inayosisitiza kipengele cha mjengeko wa kazi iliasisiwa na Ferdinand de Saussure (de Saussure, 1916). Kwa mujibu wa Habib (2005), baadaye,

nadharia hii ilishadidiwa na wataalamu kama vile Jakobson (1960), Barthes (1964) na Lévi-Strauss (1968). Katika muktadha wa kifasihi, nadharia hii huona kuwa matini ya kifasihi inafanya kazi kama mashine iliyotengezwa kwa kutumia maneno. Huiona matini hiyo kama mfumo mkuu wenye mifumo midogomidogo ndani yake. Mifano ya mifumo hiyo midogomidogo ni wahusika, dhamira, msuko wa matukio, lugha, mandhari, na mbinu za kibunilizi. Hivyo, mtunzi huchukuliwa kama fundi anayeitengeneza kazi husika ili ifanye kazi na kutoa maana fulani kwa kuzingatia uhusiano wa kimfumo.

Ifuatayo ni mihimili minne ya nadharia hii. Mosi, matini ya kifasihi hufanya kazi kama mashine iliyojengwa kimfumo. Matini hiyo ya kifasihi ni mfumo mkuu unaoundwa na mifumo midogomidogo mingi. Hivyo, maana ya matini ya kifasihi hupatikana kutokana na mfumo au mjengeko wake. Pili, neno, sentensi, alama au picha ya kifasihi haiwezi kuwa na maana moja katika kazi ya fasihi. Tatu, lugha ni kipengele cha msingi cha kazi ya fasihi. Wanaumuundo wanaamini kuwa lugha ni kibebeo cha maana ya kazi husika. Wanaongeza kuwa dunia yote inayohusu fasihi bubebwa na maneno. Hivyo, umakini kwenye uhakiki wa fasihi uwekwe katika maneno yanayounda kazi inayohusika. Nne, kuna mfungamano mkubwa baina ya lugha na utamaduni. Vipashio vya lugha huweza kuleta maana tofauti kulingana na jamii vinakotumika. Wanaumuundo huuangalia utamaduni kama mzazi wa lugha au maneno yanayounda kazi. Strauss (1968) anasisitiza kuwa tofauti za kiutamaduni inabidi zizingatiwe katika uhakiki wa kazi ya fasihi. Tano, uhakiki wa kazi ya fasihi lazima uhusishe mawazo (chukulizi) za awali.

Misingi (a) na (c) ilituongoza kubaini mbinu mbalimbali za kuwakweza wahusika katika kazi zao. Misingi (b), (d) na (e) imetumika katika kuchambua maana na mwelekeo wa jitihada za wahusika kutatua matatizo mbalimbali wakiwa wamejengwa kwa kutumia mbinu tofauti za ukwezwa. Aidha, fikra za msingi (a) zilihusishwa na za msingi (e) ili kuainisha mbinu za ukwezwaji wa wahusika kadri zilivyojitokeza katika riwaya teule.

## Methodolojia

Makala hii ni zao la uchunguzi wa kimaktaba. Data zilipatikana kupitia uchambuzi wa matini. Data zilipatikana kwa kusoma na kuchambua vipengele vinavyohusiana na mbinu za ukwezwaji wa wahusika wa riwaya teule, *Njama* (1981) na *Kamata au Ua* (2020). Riwaya hizi ziliteuliwa kwa kutumia mbinu za usampulishaji lengwa wa kimakusudi na usampulishaji lengwa wa kuzingatia ukaribu. Mbinu ya usampulishaji lengwa wa kimakusudi ilitumika kutokana na kuwa kila moja ya riwaya pendwa hizo inawakilisha muhula wake, yaani muhula wa ulimbwende ambao ulishuhudia kushamiri kwa riwaya pendwa na muhula wa usasa. Mbinu ya usampulishaji lengwa wa kuzingatia ukaribu ilitumika kuziteua riwaya hizo mbili miongoni mwa riwaya nyingi zinazowakilisha mihula tajwa. Hivyo, wakati mwandishi wa makala hii anapata wazo la kutafiti suala hili, riwaya hizi zilipatikana kwa urahisi na ukaribu katika mazingira aliyokuwapo.

Data zilizopatikana zina mwelekeo wa kitaamuli. Hivyo, zilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya usimbishaji wa maudhui. Kupitia mbinu hii, data zilizopatikana zilipangwa katika misimbo (makundi) mbalimbali iliyobeba mwelekeo mahususi wa kimaana. Kisha, maana za misimbo hiyo zilihusishwa ili kujenga maana kuu inayokidhi lengo la kubainisha mbinu za ukwezwaji wa wahusika wa riwaya pendwa za Kiswahili.

## Mbinu za Kuwakweza Wahusika wa Riwaya Pendwa ya Kiswahili

Sehemu hii inawasilisha mbinu zilizotumiwa na watunzi wa riwaya teule kuwakweza wahusika wa riwaya zao. Mbinu tano zinazojadiliwa ni kuwavisha silika ya usangwini, kutumia sadfa, kuwavisha ujuzi wa juu wa kupigana, kuwapa uwezo mkubwa wa kufikiri, na kuwapa ujuzi wa hali ya juu wa kutumia teknolojia. Uchambuzi wa namna mbinu hizo zilivyotumika katika riwaya teule unafanywa katika sehemu zinazofuata.

### Kuwavisha Silika ya Usangwini

Usangwini ni miongoni mwa vionjo vinne vya silika inayojenga haiba ya mwanadamu. Aras (2015) anabainisha silika zingine kuwa ni uflegmatiki (*phlegmatic*), umelankoliki (*melancholic*), na ukoreliki (*choleric*). Ponera & Kasiga (2019) wanaeleza kuwa watu wenye kionjo cha usangwini huwa na wingi wa kiambato cha 'haima' kinachopatikana kwenye damu. Kiambato hiki huwa na kiasi kikubwa cha hewa. Kuwapo kwa kiasi kikubwa cha hewa katika damu kunafanya miili yao kuwa na msisimko mkubwa ambao huwafanya wawe na kiwango kikubwa cha uchangamfu.

Ponera & Kasiga (*wameshatajwa*) wanabainisha kuwa vionjo vya kisilika katika fasihi hudhihirika kupitia tabia na majukumu ya wahusika katika kazi husika. Wanaongeza kuwa matendo, tabia na maamuzi wanayofanya wahusika wa kazi ya kibunilizi huendana na namna walivyojengwa kihaiba. Wahusika wenye silika ya usangwini huwa na tabia zifuatazo: Mosi, ni wasondani (huwa na tabia ya kutoficha mambo, hisia au tabia zao). Pili, huwa na kipaji kikubwa cha uongeaji na ushawishi. Tatu, ni wacheshi na hupenda kujichanganya kwenye mikusanyiko. Hivyo, huwa wepesi kutengeneza marafiki. Nne, huwa na uthubutu wa kufanya mambo

mbalimbali; hawana haya katika kufanya jambo lolote. Tano, hujiamini (hawana hofu), na hawakati tamaa. Sita, wana akili nyepesi na ya kibunifu katika kung'amua au kutatua mambo. Saba, hupenda hali ya ufutuhi (kama vile dhihaka, mafumbo, kejeli).

Katika riwaya teule, waandishi wamewavisha wahusika wao sehemu kubwa ya sifa za silika za haiba ya usangwini. Maoni yetu ni kuwa,hii ni mbinu mama ya kuwakweza wahusika wa riwaya pendwa. Hii ni kwa sababu takribani mbinu zingine zote msingi wake ni kuwapo kwa vionjo vya usangwini.

Mwandishi wa makala hii anaungana na fikra za Ponera & Kasiga (2019) ambao wanamfafanua Willy Gamba—mhusika mkuu wa riwaya zote za Aristablus Musiba, ikiwamo *Njama*—kama msangwini. Wanasema:

> Kiwajihi, Willy Gamba anajengwa katika kazi hizo kuwa na miaka takribani thelathini. Ni kijana mtanashati ... Pia, ni kijana mwenye kiwango kikubwa cha hisa ya akili (*IQ)* ... kutokana na sifa hii tunaoneshwa jinsi Willy Gamba alivyo mwepesi wa kufikiri na kujenga hoja maridhawa katika mijadala, kufikiria njia za kujinasua pale anapokuwa katika hali ngumu dhidi ya adui, pamoja na kuunganisha mambo madogomadogo ili kupata jambo kubwa na muhimu katika kuelekea katika jawabu la fumbo fulani (uk. 103).

Mafanikio ya mhusika huyu katika riwaya ya *Njama* yanatokana na sifa kama vile ucheshi, uthubutu wa kiwango cha juu, ujasiri, uzalendo, na ulumbi (uhodari wa kuongea, kujenga hoja au kushawishi). Sifa hizohizo ndizo anazisawiri Patrick Kafuku kwa Mathew Mulumbi, mhusika mkuu wa riwaya zake zote. Katika riwaya ya *Kamata au Ua*, Mathew Mulumbi na washirika wake wanapambwa na sifa za uthubutu wa kiwango kisichomithilika, ujasiri, na uzalendo.

Mathalani, waandishi wa riwaya teule wameonesha kuwa usangwini wa wahusika wao unasababisha wapendwe na kuingia kirahisi katika uhusiano wa kingono. Hii ni kwa sababu kutokea kwa uhusiano huo wa kingono kunachagizwa sana na mwonekano pamoja na wepesi wao wa kujenga hoja (kutongoza). Katika riwaya ya *Njama*, Willy Gamba anaoneshwa akipendwa na wasichana mbalimbali, ambapo baadhi yao alifikia kufanya nao ngono (uk. 7-9), kama mwenyewe anavyojigamba: "Nakuambia mimi nilizaliwa na bahati ya kuelewana na hawa watoto wa kike, maana ni mara chache sana kunichenga" (uk. 9). Hali ni hiyohiyo kwa riwaya ya *Kamata au Ua*. Katika riwaya hii, Mathew Mulumbi anatumia elementi za kisangwini kumpata mwanamke yeyote amtakaye kwa shabaha ya kimapenzi au kijasusi, kama alivyofanya kwa Silvia Mwalule, afisa wa Shirika la Ndege la Tanzania (uk. 41-42), hadi akafanikisha shabaha ya kumwokoa Rais asiuawe.

Mhimili mmojawapo wa Nadharia ya Umuundo unasisitiza kuwa kazi ya fasihi ni mfumo mkuu unaoundwa na mifumo midogomidogo; hivyo, maana ya matini ya kifasihi hupatikana kutokana na mjengeko wake. Tunaamini kuwa waandishi wa riwaya hizi teule hawajawapa wahusika wao haiba hiyo kibubusa, bali wamewavisha vionjo vya kisangwini ili waweze kuwashinda maadui zao. Fikra hii ya kimuundo inatusukuma kutoa maoni kuwa hali ya mafanikio ya wahusika hao ingekuwa tofauti kama wangevikwa vionjo vya haiba ya upole, usiri na undani kama vile silika ya uflegmatiki au umelankoliki.

Kwa kuwa tumeeleza kuwa mbinu hii huwa mama wa mbinu zingine, mdhihiriko wa kiutendaji kuhusu namna sifa hizo zinavyofanikisha

malengo ya Willy Gamba umo katika data na uchambuzi wa mbinu zinazofuata.

**Kutumia Sadfa**

Sadfa huchukuliwa kama kisawe cha neno 'bahati'. Katika muktadha wa ubunaji wa kazi za fasihi, sadfa huhusishwa na mpangilio na utokeaji wa matukio katika namna ya bahati (Vargish, 1985). Kwa mujibu wa Maffa (2020), sadfa huhusisha utokeaji wa jambo kulingana na vipengele vya wakati, mahali, mhusika/wahusika, kitendo kinachofanyika, na shabaha ya kutimia kwa jambo. Hii ni mbinu ya kibunilizi ambayo, chambilecho Vargish (*ameshatajwa*), huambatana na viashiria vya kustaajabisha ambavyo hutokea bila kuwa na uhusiano wa moja kwa moja. MacDonald (1968) anaonya kuwa, nje ya 'dunia ya kifasihi', sadfa huweza kukosa maelezo au ithibati za kisayansi juu ya utokeaji wake katika jamii.

Katika riwaya teule, mbinu hii imetumiwa na watunzi kuujenga ukwezwaji wa wahusika ili wafanikishe malengo yao. Tumekwishadokeza kuwa sadfa hutazamwa kama bahati. Wahusika wa riwaya teule wamepambwa wakiandamwa na bahati inayowawezesha kukwepa mitego na hatari au kutanzua mafumbo mazito yaliyofumbwa na maadui wao.

Katika riwaya ya *Njama*, mwandishi anadhihirisha mara kadhaa jinsi sadfa inavyofanikisha kuwinda na kutanzua fumbo linalohusiana na msako wa silaha zilizoibiwa. Mathalani, Willy Gamba na makomredi wenzake, wakiwa wanaendelea na uchunguzi wao, wanakutana na taarifa ya kutoweka kwa kichaa aliyezoeleka kuonekana nje ya ofisi yao kwa muda mrefu. Mwandishi anaeleza:

> Sijui ni mafikara yangu tu, ila limekuja kama wazo la kunishangaza … unajua pale kwenye lango la kuingia ndani ya ofisi yetu kumekuwa na mwendawazimu ambaye amekaa pale zaidi ya mwezi mzima … Alikuwa hatoki pale hata dakika moja, usiku na mchana. Leo mlipokuja alikuwepo pale … huwa anaombaomba kila mgeni anayefika pale ofisini … Sasa kitu cha ajabu ni kwamba wakati tunaondoka pale ofisini kwetu sikumwona, na wala makopo yake na kirago chake hakikuwepo. Sijui jambo hili lina maana yoyote au mnaonaje …? (uk. 74-75).

Maelezo haya yanatolewa na Magreth, mhusika ambaye mtunzi anamkutanisha na Willy Gamba na makomredi wenzake kwa kutumia sadfa iliyosanwa kiufundi. Sadfa hapa inaweza kudhihirika pale msomaji anapojiuliza kuhusu vipengele vitatu vinavyojitokeza katika nukuu hii. Navyo vinawahusisha akina Willy Gamba kufika katika ofisi hizo, kichaa aliyekuwepo ofisini hapo kwa muda mrefu kutoweka siku hiyo hiyo, na Magreth kuonana na akina Willy Gamba na kuwapa maelezo kuhusu kichaa aliyetoweka. Msomaji anaweza kujiuliza: "Ingekuwaje kama akina Willy Gamba wasingeonana na Magreth siku hiyo?" "Ingekuwaje kama, pamoja na akina Willy Gamba kuwasili ofisini pale, kichaa asingetoweka?" Au "Ingekuwaje kama Magreth asingewapa maelezo hayo kuhusu kichaa?" Kwa jicho la Nadharia ya Umuundo—kupitia mhimili unaosisitiza ulazima wa kuhusisha chukulizi fulani katika kuichunguza kazi ya fasihi—tunaamini kuwa ilisadifu tu kwa mambo yote hayo kutokea kwa pamoja ili kutimiza lengo la mwandishi kwa hadhira yake.

Imedokezwa katika ufafanuzi wa hoja iliyopita (ya usangwini) kuwa hoja hizi zingine (kama hii ya wahusika kuvikwa sadfa katika utendaji wao) zina uhusiano na sifa zinazoujenga usangwini. Mathalani, katika sadfa ya kwenye tukio hili linalowahusisha akina Willy Gamba, Magreth na kichaa,

palihitajika uwezo wa juu na wepesi wa kuunganisha matukio—hata kama yanaonekana madogo. Sifa hii iliyodhihirika kwa Magreth na Willy Gamba katika tukio hili ni ya haiba ya usangwini. Msomaji anapoendelea na vitushi vya riwaya hiyo, hatimaye, anakuja kuona kuwa sadfa hiyo ilitoa mchango mkubwa katika kufanikisha shahaba ya akina Willy Gamba.

Tukio lingine lililosanwa kisadfa linahusu mwendelezo wa mapambano baina ya Willy Gamba na timu yake dhidi ya genge la wezi wa silaha. Mwandishi anaijenga hivi sadfa yake:

> Kwenye mtaa huu wa Nkrumah niliwakaribia kabisa, nikiwa nimeacha magari mawili tu kati yangu na wao. …nadhani walikuwa wanadhani nitawafuata kwa gari langu ambalo walikuwa wanalijua sana … Walikwenda moja kwa moja na kushika Barabara ya Pugu. Walipofika njia panda ya Barabara ya Chang'ombe na Pugu, walikata kushoto na kuingia Barabara ya Chang'ombe. Saa hizi magari hayakuwa mengi barabarani, hivyo kila gari lilikwenda kasi. Nilikuwa na bahati kuwa magari yote mawili yaliyokuwa kati yangu na wao nayo yalikata na kuingia barabara hiyohiyo, hivyo kuzidi kunificha (uk. 82).

Ni sadfa tu kuwa, kwa wakati huo, Willy Gamba alikuwa anawafuata maadui wake kwa kutumia gari ambalo hawakulijua. Aidha, ni sadfa tu kuwa, kwa wakati huo, barabara haikuwa na magari mengi, hivyo, kuziwezesha pande hizi mbili zinazohasimiana kukimbizana kwa urahisi. Zaidi, ni sadfa kuwa hata magari mawili yaliyokuwa katikati ya magari ya wahusika wa pande hizi mbili zinazohasimiana nayo yalikuwa yanaelekea kulekule, kiasi cha kurahisisha maficho na mawindo ya Willy Gamba! Yamkini, bila kuwapo kwa sadfa hiyo Willy Gamba asingefanikiwa kuwafuata na kukamilisha azma yake ndiyo maana hata mtunzi amempa maneno ya moja kwa moja kuwa, "Nilikuwa na bahati kuwa magari yote mawili yaliyokuwa kati yangu na wao nayo yalikata na kuingia barabara

hiyohiyo, hivyo, kuzidi kunificha." Kulingana na Nadharia ya Umuundo ambayo huvipa thamani vipengele mbalimbali vya kazi ya fasihi kama sehemu ya mfumo mkuu, mbinu ya sadfa inajitokeza kama kipengele muhimu kinachounda uwezo wa mhusika wa riwaya.

Mwandishi wa riwaya ya *Kamata au Ua* pia ametumia mbinu ya sadfa kuwakweza wahusika wake hadi wakapata ufanisi kulingana na malengo yao. Mfano mmojawapo wa namna mbinu ya sadfa inavyojitokeza kuwakweza wahusika unaonekana wakati serikali na mamlaka za usalama zinaposaka namna ya kuwaokoa watu waliotekwa na magaidi na kushikiliwa ndani ya Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano uliopo jijini Arusha. Wakiwa katika mjadala wa namna ya kuwakabili magaidi, inakuja amri kutoka kwa magaidi kuwa serikali itume madaktari wawili kwenda ndani ya ukumbi huo ili kuwatibu mateka. Serikali inaamua kutumia mwanya huo kupenyeza majasusi badala ya madaktari ili wakafanye kazi mbili—kutibu majeruhi na kupeleleza jinsi ya kuwaokoa mateka wote. Katika msako wa watu hao wawili wenye sifa ya kuwa matabibu, ndipo sadfa inapojitokeza. Mwandishi anasimulia:

> Huo unaonekana ni mpango mzuri sana. Kuna mtu anaitwa Agai Sempa. Ni jasusi ambaye alikuwa katika kizuizi kwa kosa la kuharibu misheni. Mathew aliniletea faili lake na kuomba aachiwe. Leo nililipitia faili lake nikaelekeza aachiwe huru. Tayari amefika hapa ikulu. Nilikuwa na mpango wa kumtumia katika kazi nyingine, lakini kwa kuwa imejitokeza kazi hii, basi ataungana na Gosu Gosu kwenda Arusha katika hiyo misheni (uk. 52).

Rais anapata wazo hili la kumtumia Agai Sempa wakati yeye, kama amirijeshi, na wasaidizi wake wako katika hali hiyo ya msawajiko kutokana na tukio hilo la ugaidi. Wakiwa hawajui aliko Mathew Mulumbi ambaye wanategemea angewanasua katika mazingira kama haya, imesadifu tu kuwa

kuna mtu mwingine mwenye sifa zinazoendana na za Mathew Mulumbi au Gosu Gosu. Mtu huyo aliyewekwa kizuizini ametolewa siku hiyohiyo. Bahati nyingine ni kwamba, wakati huo walipokuwa wanaongea, tayari alikuwa ndani ya viunga vya ikulu. Bahati zaidi ni kwamba, alipoelezwa tu kuhusu kushiriki katika misheni hiyo ya hatari, alikubali mara moja! Hii ni sadfa ya kiwango cha juu.

Mwandishi amewakutanisha 'kibahati' Gosu Gosu na Agai Sempa ili wapate fursa ya kushirikiana kwenda ndani ya ukumbi huo wenye hatari. Wakiwa ndani ya ukumbi, wahusika hawa wanashirikiana kwa weledi na kuwaua magaidi takribani ishirini, hatimaye kuwaokoa mateka.

Vilevile, kwa shabaha ya kukamilisha lengo lake, mwandishi ametengeneza sadfa ya majasusi hao wawili kukutana na mtu waliyekuwa wamempa kipaumbele cha kumsaka baada ya kuingia ndani ya ukumbi. Mwandishi anasema:

> Gosu Gosu akamfuata yule jamaa waliyempasua paja. Hakuwa na nguvu ... Akamtikisa kisha kumsemesha kwa lugha ya Kifaransa: "Wewe ni nani? Niambie tafadhali. Tuko hapa ili kuwaokoa." Alisema Gosu Gosu.
>
> "Fa…Fa.." akanyamaza … akakohoa kidogo. "Fabrice Kayembe," hatimaye alisema jamaa yule kwa sauti ya chini sana (uk. 64).

Hii ilikuwa baada ya madaktari hao bandia kumaliza kufanya upasuaji wa mgonjwa ambaye alikuwa mmoja wa mateka pamoja na kuwaua magaidi waliokuwa wanasimamia upasuaji huo. Katika mfululizo wa usimulizi wa vitushi vya riwaya hii, Fabrice Kayembe ni mhusika anayeshikilia kiini cha sababu za kutokuwapo kwa amani katika nchi za Maziwa Makuu. Hivyo, akawa kwenye orodha ya watu wa muhimu mno waliokuwa wanasakwa na

majasusi waliokuwa wanapeleleza kuhusu sakata hilo. Kitendo cha majasusi kujikuta kumbe waliitwa kumfanyia upasuaji mtu ambaye nao walikuwa wanahaha kumsaka ni cha sadfa. Ni kupitia sadfa hii, majibu mengine mengi yalipatikana kuhusu sakata hilo, hivyo, kuwapa pia sifa (kuwakweza) wahusika walioshiriki kupeleleza jambo hilo.

Kuhusu kufaa au kutofaa kwa Agai Sempa katika shughuli ya ujasusi, mwandishi anatumia kinywa cha Gosu Gosu akimpa sifa ya Agai Sempa kwa kusema:

> … njiani wakati (Gosu Gosu) akipanda kueleka katika paa, akakutana na damu iliyotapakaa chini. Akatabasamu kisha akaendelea na safari akijisemea: "Nashukuru tumepata nguvu mpya katika timu yetu. Huyu Agai ni mtu anayetufaa sana. Nimependa ufanyaji kazi wake" (uk. 72).

Hii ni nukuu ya kumkweza Agai Sempa ambaye alipatikana kwa sadfa tu. Msomaji anapoendelea kusoma riwaya hii, anabaini kuwa mhusika huyu aliyepatikana kisadfa anakuja kutoa mchango mkubwa sana katika kukombolewa kwa watu waliotekwa na magaidi. Kwa ujumla, mwandishi amewapa wahusika hawa kiwango cha juu cha ujasiri na uthubutu. Katika hali ya kawaida, si rahisi mtu kukubali kwenda kuingia katika ukumbi wenye magaidi wenye silaha tena huku akijua kuwa hakidhi sifa za mtu anayehitajika na magaidi hao.

Vilevile, katika riwaya ya *Kamata au Ua*, mbinu ya sadfa inatumika kumsaidia mhusika Maurine Kyaso katika kupanga na kutekeleza njama za kuiangamiza nchi ya Tanzania. Rais anamteua Maurine Kyaso kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Siri ya Usalama wa Taifa bila kujua kuwa huyo ni mwanawe aliyemzaa zama za ujana wake na kuwatelekeza yeye (mtoto) na mama yake. Mwandishi anasema:

> …ulimwacha Amira akiwa na mimba yako. Ukaondoka kimyakimya. Alipojifungua alijaribu kukutafuta, lakini ulimkana na kutishia kumuua… mtoto ambaye ulimkana ni mimi. Kifo cha mama yangu kiliniumiza sana. Niliweka ahadi ya kuhakikisha siku moja ninalipa kisasi kwako na kwa Tanzania … (uk. 255 - 256).

Mtoto huyu ambaye baadaye alikuja kushika nafasi nyeti ya usalama wa nchi kisadfa, alijawa na chuki dhidi ya nchi nzima ya Tanzania kutokana na kutelekezwa. Hivyo, kutokana na kushika nafasi nyeti ya kiusalama, akaja kuwa kiungo madhubuti wa kufanikisha hila za mabeberu katika nchi ya Tanzania. Kulingana na Nadharia ya Umuundo, sadfa hii ni sehemu ya mifumo midogomidogo inayounda mfumo mkuu ambao ni riwaya yenyewe. Kwa kuwa nadharia hii huamini kuwa matini ya fasihi hufanya kazi kama mashine, ni wazi kuwa sadfa hii ni kijenzi kilichopachikwa kwa makusudi ili kumpamba mhusika kiuwezo na, hatimaye, kukamilisha lengo la mtunzi. Nadharia hii inayakinisha maoni yetu kuwa kufanikiwa kwa Maurine Kyaso katika kutekeleza hila za mabeberu (ambazo kwake alizitumia kama mpango wa kulipa kisasi) kulitokana na sadfa iliyomweka katika nafasi ya kuongoza idara nyeti ya usalama.

**Kuwapa Uwezo wa Kutafakari Kitunduizi**

Tung & Chang (2009) wanabainisha kuwa, mbali na kuwa na stadi-mango kama vile kuweza kuchora, kucheza, au kutafsiri, ni muhimu mtu yeyote kuwa na stadi-laini mbalimbali. Hii ni kwa sababu stadi-laini hizo humwezesha mtu huyo kumudu maisha. Miongoni mwazo ni tafakuri tunduizi. Kwa mujibu wa Kim (2011), tafakuri tunduizi ni stadi inayohusisha kufikiri jambo kwa kina kwa kuhusisha vipande vya ithibati au viashiria vinavyotambuliwa na milango ya fahamu. Tosuncuoglu (2018) anaeleza kuwa tafakuri tunduizi huchukuliwa kama msingi wa kufanya

uamuzi sahihi. Kutokana na umuhimu huo, Kim (*ameshatajwa*) anasisitiza kwamba stadi ya tafakuri tunduizi inapaswa kupewa kipaumbele katika mifumo ya elimu ya karne ya 21.

Waandishi wa riwaya teule wamewavisha wahusika wao uwezo mkubwa wa kufanya tafakuri tunduizi kama sehemu ya mbinu za kuwakweza. Katika riwaya ya *Njama*, Musiba anamsawiri Willy Gamba kama kiumbe mwenye uwezo wa kipekee katika kufanya tafakuri za kidadisi na kitatuzi. Yako matukio mengi yanayothibitisha jambo hili. Katika tukio mojawapo, mwandishi anasema:

> "Jaribu kukumbuka," nilimwambia, "wakati marehemu anakueleza uweke zile karatasi za kuchukulia silaha kulikuwa na mtu mwingine yeyote?"
>
> Alikaa kimya kwa muda, kisha akajibu, "Hapana." Halafu kama amegutuka akasema, "Ndiyo nakumbuka sasa, alikuwepo tarishi wetu wa hapa ofisini." Nikasikia kengele ya tahadhari inalia kichwani mwangu (uk. 69).

Upelelezi na ujasusi hujiegemeza sana katika kutafakari na kuunganisha vitu au viashiria vinavyoonekana kuwa vidogo au havina maana. Katika tukio lililonukuliwa hapo juu, Willy Gamba anatumia akili kufanya tafakuri na kuunganisha dhana ili kupata jibu. Elementi za namna hiyohiyo zinaonekana tena wakati Willy Gamba, ambaye katika riwaya hii ni mhusika-msimulizi, anasimulia:

> Habari kama hizi ndizo huwa zinanitibua, maana wakati kifo kinatokea halafu kinatokea kitu kingine chenye uhusiano wa karibu namna hii, basi hapo ndipo huwa naanza kujumlisha moja kwa moja na kupata mbili (uk. 70)

Cheche na cheche huzaa moto! Hatimaye, tafakuri ya Willy Gamba ya 'kujumlisha moja na moja' ilizaa matunda kwa kufanikiwa kutumia fikra

hizo kupata majibu ya msako wake wa wezi wa silaha za ukombozi wa Bara la Afrika. Kulingana na Nadharia ya Umuundo, kupitia mhimili unaothamini vipengele mbalimbali vya kazi ya fasihi kama sehemu muhimu zinazojenga mfumo mkuu, sifa ya wepesi wa kiakili inajitokeza kama kipengele muhimu kinachounda uwezo (wa kipekee) wa mhusika huyu.

Katika riwaya ya *Kamata au Ua*, mwandishi pia amewapa wahusika wake uwezo wa juu wa kufikiri na kutatua changamoto mbalimbali kwa wepesi. Hali hii inabainika katika mchakato wa kuwasaka magaidi na mabeberu wenye nia mbaya. Tukio mojawapo linalodhihirisha namna mbinu ya fikra tunduizi inavyotumika kuwakweza wahusika wa riwaya pendwa ni kitendo cha kishujaa walichokionesha Gosu Gosu na Agai Sempa kukubali kujipeleka kwa magaidi wakijifanya madaktari. Mwandishi anasimulia:

> "Fanya haraka haraka!" Alisema kiongozi wa magaidi. Gosu Gosu hakujua aanzie wapi. Akakohoa mara tatu kuashiria kuhitaji msaada kutoka SNSA (Idara ya Siri ya Usalama wa Taifa). Daktari wa SNSA aliyekuwa akiwapa maelekezo, akaanza kumpa maelekezo ya kufanya (kupitia vifaa vya mawasiliano walivyobandikwa kwa siri katika ngozi zao). Gosu Gosu akaanza upasuaji. Wakati akifanya upasuaji, jamaa aliyekuwa anapasuliwa aliuma meno kwa maumivu makali aliyoyahisi. Gosu Gosu hakumjali akaendelea na upasuaji. Kiongozi wa magaidi alikuwa amesimama pembeni ya Gosu Gosu, akishuhudia kinachoendelea (uk. 59, ufafanuzi kwenye mabano ni wa mwandishi wa makala hii).

Hapa, Gosu Gosu, ambaye katika muktadha huu amejifanya daktari wa upasuaji, anafanikiwa kufanya upasuaji kupitia maelekezo yanayofanywa kwa siri kwa kutumia teknolojia kutoka kwa jasusi mwenziwe ambaye ni daktari aliyekuwa ofisini. Nadharia ya Umuundo inasisitiza kuwa lugha ni kipengele cha msingi cha kazi ya fasihi kwa sababu ndiyo kibebeo cha maana ya kazi husika. Katika nukuu hii, tunaona 'lugha ya kijasusi'

(kukohoa mara tatu) ikitumika. Tulipoweka makini kwenye kuhakiki namna hii ya kuwasiliana—kama tunavyosisitizwa na mhimili huu wa Nadharia ya Umuundo—tulibaini kuwa mawasiliano yaliyofanyika hadi kufanikisha upasuaji huo yamewezeshwa na tafakuri tunduizi, vinginevyo, bila shaka, Gosu Gosu na Agai sempa wangegundulika kuwa si madaktari; hivyo, wangeuawa.

Tukio lingine ambalo wahusika wa riwaya ya *Kamata au Ua* wamejengwa kwa sifa ya kutumia tafakuri tunduizi katika kutatua matatizo yanayowakabili linahusu utanzuaji wa lugha-fiche waliyokuwa wanatumia maadui. Mwandishi anasema:

> Ruby akaendelea kubofya kompyuta, sekunde chache baadaye, yakaanza kusikika mazungumzo yao.
> "*Thirteen, one, seven*," ilisema sauti ya mwanamke.
> "*One, four, seven, zero*," ilisema sauti ya mwanaume ambayo waliamini kuwa ni sauti ya Joseph.
> "*Two*." alisema mwanamke.
> "*Two*." alisema pia Joseph na simu ikakatwa. Wote wakabaki wanatazamana. Rais likamtoka cheko dogo la mshangao (uk. 152).

Haya ni maongezi ya maadui (Mwasi na Joseph) ambayo Gosu Gosu na Ruby waliyanasa. Katika hali ya kawaida, maongezi haya yanayotumia lugha-fiche ya kijasusi yanaonekana kama yasiyo na maana, ndiyo maana hata waliokuwa wanayasikiliza waliishia kucheka kwa mshangao. Mhimili wa Nadharia ya Umuundo unaosisitiza kuwa lugha ni kipengele cha msingi cha kazi ya fasihi ulituongoza kubaini kuwa maneno hayo hayakutumika kimakosa. Mwandishi amewajenga wahusika wake kama watu wenye kufanya tafakuri katika utendaji wa mambo yao. Ni wazi kuwa Mwasi na Joseph walifanya tafakuri ya kina ili kuunda namba hizo walizozitumia kama misimbo ya mawasiliano yao kwa lengo la kujificha. Ili kupata maana

ya maongezi haya, iliwapasa Ruby na Gosu Gosu nao kufanya tafakuri tunduizi. Ulazima wa wahusika hawa kutunduwia mawasiliano hayo unayakinishwa na mhimili wa Nadharia ya Umuundo unaosisitiza kuwa neno, sentensi, alama au picha ya kifasihi haiwezi kuwa na maana moja katika kazi ya fasihi. Waliamini kuwa lazima kuna maana inafichwa katika mawasiliano hayo. Hatimaye, kupitia utunduizi walioufanya, walifanikiwa kuelewa maudhui ya misimbo hiyo—ambayo ni sehemu ya njama za maadui za kuisambaratisha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Kuwapa Ujuzi wa Hali ya Juu wa Kupigana**

Mbinu nyingine waliyotumia waandishi wa riwaya pendwa teule kuwakweza wahusika wao ni kuwavisha uwezo wa juu wa kupigana kwa kutumia viungo vya mwili au kwa kutumia silaha. Ujuzi huo huwasaidia kuvuka vikwazo mbalimbali wawapo katika mchakato wa kuyafikia malengo yao. Waandishi wa riwaya zote mbili wametumia mbinu hii.

Katika riwaya ya *Njama*, takribani wahusika wote wamepewa na mwandishi uwezo wa juu wa kupigana. Katika tukio mojawapo, mwandishi anatueleza kupitia sauti ya Willy Gamba mwenyewe. Anasema:

> "Simama," alisema Lukas.
> Sikusimama. Basi walinijia wote pale kitini kama faru, na mimi Willy tayari nilikuwa nawashwa kumwonyesha huyu mkubwa wao kuwa Willy hasukumwi ovyo … Kama umeme, nilisimama upesi na kukwepa ngumi ya Lukas na kwa sababu alikuwa ameitupa kwa nguvu sana alipepesuka, mimi nikampiga teke kwenye map*mbu akalia kama nguruwe … (uk. 93, neno lililowekewa nyota na mwandishi wa makala hii ili kujenga tasifida linamaanisha sehemu ya via vya uzazi vya mwanamume).

Tukio linalosawiriwa katika nukuu hii linamhusisha Willy Gamba akikabiliana na watu wanne wenye silaha na kuwashinda. Hapa, tunaoneshwa jinsi Willy Gamba alivyo hodari katika kutumia viungo vyake vya mwili kuwapiga na kuwashinda maadui. Vilevile, mwandishi anamkweza Willy Gamba kwa kumpa uwezo wa ajabu wa kujiokoa dhidi ya risasi za maadui. Anasema:

> …nikawaona Max na yule kijana mwingine karibu kabisa na mimi wameinua bastola tayari kufyatua. Nilijiviringisha hewani namna ambayo hata wao walishangaa; risasi zao zote zikanikosa. Wakati uleule nikaachia za kwangu nikawapata wote nao wakaanguka chini (uk. 170)

Kwa hakika, uwezo aliovikwa Willy Gamba katika matukio haya umetiwa chumvi ili mwandishi atimize lengo lake. Huu ni ukwezwaji kwa sababu umevuka uwezo wa kawaida wa mwanadamu.

Katika riwaya ya *Kamata au Ua*, mwandishi anaitumia mbinu hii ya kuwakweza wahusika wake kwa kuwavisha uhodari wa kupigana kupitia Gosu Gosu na Agai Sempa. Katika tukio mojawapo ambalo linawakweza wahusika hawa kwa kutumia mbinu hii, mwandishi anasema:

> Kuna nini hapa mbona ha..." alisema gaidi lakini hakumaliza sentensi yake. Mkono wa Gosu Gosu uliinuliwa kwa kasi ya umeme na kuzamisha mkasi katika koo lake mara tatu. Kilikuwa kitendo cha ghafla, damu zikaruka. Kwa mikono yenye nguvu, akakikamata kichwa cha yule gaidi na kuivunja shingo. Kwa taratibu na ustadi mkubwa, akamlaza chini. Wakati akimlaza chini yule gaidi, Agai naye alikuwa amemaliza kazi ya kumkata pumzi yule gaidi mwingine. Kilikuwa kitendo cha haraka mno ambacho wale magaidi hawakuwa wamekitegemea. Hawakujua kama madaktari wale walikuwa watu hatari (uk. 63).

Katika tukio hili, Gosu Gosu na Agai Sempa walikuwa pamoja katika zoezi la kumfanyia upasuaji mmojawapo wa mateka wa magaidi. Licha ya

kulindwa barabara, walipopata mpenyo mdogo tu walipambana ili kujiokoa wao wenyewe. Kisha, huo ukawa mwanzo wa kuwaokoa mateka wote. Yapo matukio mengi ya jinsi hii kuhusu uhodari wa Gosu Gosu katika kupigana. Kwa upande wa Agai Sempa, pia yako matukio kadhaa yanayomkweza kupitia uhodari wa kupigana. Tukio mojawapo linalomhusu yeye linasema:

> Agai akaanza kukohoa tena mfululizo. Mlango ukafunguliwa. Akaingia gaidi mmoja. Akamuona Agai akitetemeka, akadhani anakata roho. Hilo likamzubaisha gaidi. Akamfuata na kumfungua pingu alizokuwa amefungwa mikononi. Ghafla, Agai akageuka kama mbogo. Akamtandika gaidi kichwa kizito, akapepesuka. Hakumpa nafasi, akamuongeza tena ngumi mbili mfululizo. Gaidi akahisi kizunguzungu. Kwa kasi ya ajabu, akamgeuza na kumkaba kabali nzito. Gaidi akajitahidi kufurukuta, lakini taratibu akaanza kulegea. Agai akamuachia, gaidi akaenda chini kama furushi (uk. 118).

Hili ni pigano linalofanyika wakiwa ndegeni. Wakiwa angani, Agai Sempa anajaribu kupambana na magaidi waliokuwa ndegeni na kuwashinda. Yumkini, msomaji anaweza kustaajabia ujasiri na uwezo mkubwa wa Agai. Hata hivyo, tukiongozwa na Nadharia ya Umuundo, kupitia mhimili unaovithamini vipengele mbalimbali vya kazi ya fasihi kama sehemu muhimu ya kujenga maana ya jumla ya kazi, tunaamini kuwa mwandishi amempamba Agai Sempa kwa mbinu hii ili kuukweza uwezo wake.

### Kuwapa Ujuzi Mkubwa wa Kutumia Teknolojia

Ujuzi wa kutumia teknolojia katika kufanya upelelezi au ujasusi ni mbinu nyingine waliyotumia waandishi wa riwaya pendwa teule kuwakweza wahusika. Riwaya ya *Kamata au Ua* ina matukio mengi yanayohusisha matumizi ya teknolojia kuliko riwaya ya *Njama*. Baadhi ya nyenzo za

kiteknolojia ambazo mwandishi amezitumia kuwakweza wahusika wake ni simu za mkononi, kompyuta, kamera, ndege zisizo na rubani (*drone*), vifaa vya kusikilizia, satelaiti, na rada. Hoja yetu hapa ni kwamba, nyenzo hizi zimewaongezea uwezo wahusika katika kutekeleza majukumu yao, hivyo kuibuka na ushindi kulingana na malengo ya mwandishi.

Tukio mojawapo ambalo mwandishi wa riwaya ya *Kamata au Ua* amewakweza wahusika wake kupitia teknolojia linawahusisha wahusika wa kitengo cha TEHAMA, wakiongozwa na Ruby. Wakati majasusi pamoja na Rais wanaendelea kuwafuatilia Gosu Gosu na Agai Sempa wakiwa wanaelekea katika jengo hilo, unaibuka wasiwasi wa kukamatwa kwao. Wasiwasi huo unaelekezwa kwenye vifaa vilivyofungwa katika miili yao ili kusaidia mawasiliano. Mwandishi anatueleza:

> "Vipi kama wakigundua kamera iliyofungwa mwilini mwa Agai?" Rais aliuliza. Hakuna aliyemjibu … vile vifaa vya mawasiliano walivyowekwa masikioni havikuweza kuonekana kutokana na kufunikwa na ile ngozi maalumu iliyochukua rangi ya ngozi ya mwili (uk. 57).

Ubunifu huu wa kuficha vifaa vya mawasiliano kwa kufunika na ngozi ni matokeo ya uwezo wa juu wa Ruby katika teknolojia ya kijasusi. Pamoja na tahadhari zote ambazo magaidi walizichukua kwa kuwakagua akina Gosu Gosu na Agai Sempa, ikiwamo kuwaacha uchi wa mnyama na kuchoma moto nguo na vitu vyao vyote, mwandishi anatuonesha kuwa bado majasusi hao walifanikiwa kuingia na vifaa vya mawasiliano vilivyopachikwa katika miili yao kwa kutumia teknolojia hiyo. Kwa mtazamo wa Nadharia ya Umuundo, matumizi ya nyenzo hizi za kiteknolojia ni mfumo mdogo ulioundwa ili kuujenga mfumo mkuu ambao ni riwaya nzima. Maana tunayoipata hapa ni kwamba wahusika, hususani akina Ruby, wana uwezo wa kupambana na vikwazo mbalimbali ili kufikia kilele cha malengo yao.

Mbinu hii ya kumkweza Ruby kupitia uwezo wa kutumia nyenzo za teknolojia imetumiwa tena katika riwaya hii kupitia dhana ya udukuzi wa mawasiliano. Mwandishi anasema:

> Dakika mbili baada ya Ruby kuondoka, kukatokea mlio fulani katika simu yake. Chapchap akaweka kifaa sikioni. Akabonyeza sehemu katika simu yake na kuanza kusikiliza mazungumzo.
> "Maurine, nipe taarifa!" ilisikika sauti ya Rais Jenerali Pius.
> "Mheshimiwa Rais, tayari Ruby amekwishaondoka. Nimepokea taarifa kutoka kwa watu wangu niliowaweka kumfuatilia Ruby kama ulivyoelekeza," akasema Maurine.
> Ruby akastuka.
> "Kumbe Rais ndiye alielekeza tuchunguzwe," alishangaa Ruby (114).

Nukuu hii inaonesha kuwapo kwa teknolojia ya udukuzi wa simu ili kufuatilia mawasiliano ya mhusika bila yeye kujua. Wakati Ruby anafuatiliwa kwa maagizo ya Rais, naye anatumia ujuzi wake wa kompyuta kudukua simu za hao wanaomfuatilia. Kadiri msomaji anavyoendelea kusoma riwaya hii, anabaini kuwa mwandishi alimpa Ruby ushindi katika pambano hili la kudukuana ili, baadaye, afanikishe lengo kuu la kukamatwa kwa magaidi na mabeberu waliokuwa na hila na nchi za Afrika Mashariki.

## Hitimisho

Makala hii imejadili mbinu za kuwakweza wahusika wa riwaya pendwa za Kiswahili. Mbinu zilizowasilishwa ni tano: kuwavisha silika ya usangwini, kutumia sadfa, kuwavisha ujuzi wa juu wa kupigana, kuwapa uwezo mkubwa wa kufikiri, na kuwapa ujuzi wa hali ya juu wa kutumia teknolojia. Imedhihirika kuwa mbinu nne kati ya tano zimetumiwa na waandishi wa riwaya zote mbili zilizotafitiwa. Mbinu moja ambayo ni ya kuwapa ujuzi wa hali ya juu wa kutumia teknolojia katika kuendesha upelelezi

imetumiwa na mwandishi mmoja—wa riwaya ya *Kamata au Ua* ambayo ni ya muhula wa sasa. Hali hii ya mwandishi Patrick C. Kafuku kutumia nyenzo hizi za teknolojia ya kisasa katika kufanya ujasusi na upelelezi katika riwaya yake ya *Kamata au Ua* inatokana na ukweli kuwa muhula huu wa usasa unaenda sambamba na mapinduzi ya nne ya viwanda ambayo mkito wake mkubwa uko kwenye matumizi ya mifumo ya kidijiti katika kuendesha masuala mbalimbali duniani. Hivyo, Patrick Kifuku na waandishi wengine wa riwaya pendwa za kisasa wanaenda pamoja na mwondoko huo wa kiteknolojia. Hii ndiyo sababu ya mbinu hii kutoonekana katika riwaya za mihula iliyopita kama vile *Njama*. Hivyo, hii ni ithibati ya wazi kuwa fasihi huendana na hali halisi ya jamii inayohusika.

Makala hii imeshughulikia kipengele kimoja—mbinu za kuwakweza wahusika—katika riwaya pendwa ya Kiswahili. Kwa kuwa mkondo huu (au wa riwaya kwa ujumla) una vipengele vingi, makala inapendekeza tafiti zingine zifanywe kuhusiana na vipengele vingine, kama vile naratolojia (sayansi ya usimulizi wa vitushi vya riwaya).

**Marejeleo**

Aras, G. (2015). Personality and Individual Differences: Literature in Psychology - Psychology in Literature. *Procedia - Social and Behavioral Sciences*, 185, 250-257.

Barthes, R. (1964). *Elements of Semiology*. New York: Hill and Wang.

de Saussure, F. (1916). *Course of General Linguistic*. New York: Columbia University Press.

Habib, M.A.R. (2005). *A History of Litarary Criticism*. Malden, USA: Blackwell Publishing

Hacht, A.M. and Hayes, D.D. (2009). *Gale Contextual Encyclopedia of World Literature*. New York: Gale Cengage Learning

Jakobson, R. (1960). 'Linguistics and Poetics', in T. Sebeok (ed.), *Style in Language* (kur. 350-377). Cambridge: MIT Press.

Jumanne, A. (2018). *Mabadiliko ya Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya Kiswahili: Ulinganisho wa Riwaya za Shaaban Robert na Said A. Mohamed* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Kafuku, P.C. (2020). *Kamata au Ua*. Arusha: Joystan Tanzania.

Khamis, S.A.M. (2007). Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili. *Kioo cha Lugha*, 5, 23-31.

Kim, K.H. (2011). The Creativity Crisis: The Decrease in Creative Thinking Scores on the Torrance Tests of Creative Thinking. *Creativity Research Journal*, 23(4), 285-295.

Lévi-Strauss, C. (1968). *Structural Anthropology* [1958], Translated by Claire Jacobson and Brook G. Schoepf. London: Allen Lane.

MacDonald, W. (1968). Coincidence in the Novel: A necessary Technique. *Journal of English of National Council of Teacher of English.* 29(5), 373-388. http://doi.org/10.2307/374100

Madumulla, J.S. (1993). Mwandishi wa Riwaya ya Kiswahili na Suala la Ukweli wa Maisha. Katika *Fasihi, Uandishi na Uchapaji: Makala ya Semina ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania* (kur. 141-153). Dar es Salaam: UWAVITA.

Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Nairobi: Mture Educational Publishers Ltd.

Maffa, E. (2020). *Matumizi ya Sadfa katika Riwaya Pendwa: Mifano kutoka Kivuli, Kikosi cha Kisasi na Hofu* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Mlacha, S.A.K. & Madumulla, J.S. (1995). *Historia na Maendeleo ya Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: DUP.

Musiba, A.E. (1981). *Njama*. Dar es Salaam: Continental Publishers.

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ponera, A.S. & Kasiga, G.A. (2019). Mdhihiriko wa Kionjo cha Usangwini kwa Mhusika Willy Gamba katika Riwaya ya *Njama*. *Kioo cha Lugha*, 17, 99-113.

Senkoro, F.E.M.K. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Tosuncuoglu, I. (2018). Importance of Assessment in ELT. *Journal of Education and Training Studies*, 6(9), 163-167. Inapatikana katika http://doi.10.11114/jets.v6i9.3443

TUKI (2001). *Kamusi ya Kiswahili-Kiingereza*. Dar es Salaam: TUKI.

Tung, C.A.J. na Chang, S.Y. (2009). Developing Critical Thinking through Literature Reading. *Feng Chia Journal of Humanities and Social Sciences*, 19, 287-317.

Vargish, T. (1985). *The Providential Aesthetic in Victorian Fiction.* Charlottesville: U P of Virginia.